

MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE TANZANIA



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

KUHUSU WAGENI 16 WALIOINGIA NCHINI KUPITIA JENGO LA WATU MASHUHURI (VIP LOUNGE)

Tarehe 31/07/2017 chombo kimoja cha habari kilitoa taarifa za upotoshaji kwamba wageni 16 wenye uraia wa Lebanon, Pakistani na Somalia walinaswa katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) baada ya kupita Jengo la Watu Mashuhuri (VIP).

Taarifa sahihi za suala hili ni kwamba Tarehe 30/07/2017 abiria wanne (4) Raia wa Taifa la Pakistan waliwasili kwenye Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) na kupita Jengo la Watu Mashuhuri (VIP Lounge) ambapo nyaraka zao za safari zilikaguliwa na Maafisa wa Uhamiaji na baada kuruhusiwa kuingia nchini baada ya kujiridhisha kuwa ni halali. Abiria hao walikuwa na kibali kinachowaruhusu kutumia ukumbi wa watu mashuhuri (VIP) kilichotolewa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa.

Utaratibu uliopo katika matumizi ya Ukumbi wa watu Mashuhuri (VIP Lounge) JNIA ni kwamba wageni wote toka nje ya nchi wanaohitaji kutumia ukumbi huo wanalazimika kuomba kibali Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa na Wizara husika inapojiridhisha na vigezo vya waombaji, hutoa vibali hivyo.

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) inatoa wito kwa vyombo vya habari nchini kuandika habari kwa weledi na kuhusisha pande zote zinazohusishwa katika taarifa zao mbalimbali, ili kuepuka mkanganyiko na upotoshaji kwa jamii kwa jambo husika.

TAA ipo tayari kutoa ushirikiano kwa chombo chochote cha habari kinachowasiliana nacho kutaka ufafanuzi wa jambo fulani, ili waweze kuandika kwa umakini na ufasaha zaidi.

IMETOLEWA NA:

**KAIMU MKURUGENZI MKUU WA MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE TANZANIA
(TAA)**

BW. SALIM MSANGI